

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU



Zanzibar

20 Machi, 2025

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan anatarajia kufanya ziara ya kikazi katika Jamhuri ya Namibia kesho tarehe 21 Machi, 2025 kuhudhuria sherehe za uapisho wa Rais Mteule wa nchi hiyo Mhe. Netumbo Nandi-Ndaitwah.

Rais Dkt. Samia amealikwa kama Mgeni Rasmi na anatarajia kuhutubia kwenye sherehe hizo za uapisho zitakazofanyika sambamba na Maadhimisho ya Miaka 35 ya Uhuru wa Namibia.

Mahusiano baina ya Tanzania na Namibia ni ya kidugu na kihistoria ambayo yaliasiwa na Hayati Julius Nyerere na Hayati Sam Nujoma kipindi cha harakati za ukombozi wa nchi za Kusini mwa bara la Afrika.

Mahusiano haya yameendelea kukuzwa na kulelewa na Viongozi wote Wakuu waliowafuatia katika nyanja mbali mbali.

Mbali na kuhudhuria sherehe hizo Rais Dkt. Samia atapata fursa ya kusalimiana na mwenyeji wake na kufanya mazungumzo ya kukuza na kuimarisha mahusiano.

Kwa mara ya kwanza Namibia itapata Rais Mwanamke hivyo kufanya idadi ya Marais Wanawake barani Afrika kuwa wawili akiwemo Rais Dkt. Samia.

A blue ink signature of Sharifa B. Nyanga.

Sharifa B. Nyanga
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu



Ikulu Mawasiliano / ikulu_mawasiliano /
ikulu Tanzania / ikulu Tanzania /
ikulumawasiliano / ikulu Tanzania / ikulu Tanzania

